TANGAZO LA SERIKALI NA. 453 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA MLIMA RUNGWE YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 963 la 2019

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA RUNGWE


MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA MLIMA RUNGWE

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 24680.5 au Kilometa za Mraba 246.805

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi iliyohifadhiwa ndani ya mipaka ya Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe lililoainishwa katika Jedwali lililopo katika Ramani Jb 2876 lenye ukubwa wa Hekta 13652 ya mwaka 2013 (Skeli 1:25,000), Msitu wa Hifadhi wa Taifa Poroto Ridge ulioainishwa katika Jedwali lililopo katika Ramani Jb 2932 lenye ukubwa wa Hekta 9746 au Kilometa za Mraba 97.46 ya mwaka 2018 (Skeli 1:20,000) na Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sawago ulioainishwa katika Jedwali lililopo katika Ramani Jb 2987 lenye ukubwa wa Hekta 816.48 au Kilometa za Mraba 8.16 ya mwaka 2019 (Skeli 1:10,000):

*Tangazo La Serikali Na. 453 (Linaendelea)*




Jb 2876

---

Dodoma, ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
___24 Mei, 2024 *Waziri wa Maliasili na Utalii*